**JAMHULI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA MTWARA**

***NAMBA ZA SIMU***
***Mkuu wa Shule 0788590514***
***Makamu Mkuu wa Shule (Utawala) 0759516187***
***Makamu Mkuu wa Shule (Taaluma) 0786804745***
***Mwalimu wa Malezi (Matron) 0653952587***

***SHULE YA SEKONDARI MUSTAFA SABODO, S.L.P 158 MTWARA***

MZAZI/MLEZI WA: ……………………………………………………………

**YAH; MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO (V) KATIKA SHULE YA SEKONDARI MUSTAFA SABODO MWAKA ……………..**

Tafadhali rejea somo tajwa hapo juu

Ninayo furaha kukufahamisha kuwa mtoto wako …………………………………………………………

Ni miongoni mwa wanafunzi wachache waliopata fursa ya kuendelea na masomo ya kidato cha tano katika Shule ya sekondari Mustafa sabodo, hongera sana kwa fursa hiyo. Kwa barua hii nakuletea fomu ya kujiunga na Shule ya Sekondari Mustafa sabodo kwa mwanao.

Tafadhali nakuomba wewe na mwanao msome maelekezo haya kwa kina na kisha mkamilishe yale yote yanayotakiwa. Pamoja na kuyasoma kwa kina naomba uendelee kumshauri mwanao juu ya kutumia nafasi hii aliyoipata vema ili lengo na azma yake itimie. Nakutakia maandalizi mema na karibu sana Mustafa Sabodo Sekondari.

**MKUU WA SHULE**

## MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE

Ninayo furaha kukufahamisha kuwa mwanao ......................................................... amechaguliwa kujiunga na kidato cha tano (V) kwa mchepuo wa **EGM, HGE, HGK, HGL, HGLi na HKL** katika shule ya sekondari Mustafa Sabodo. Anatakiwa aripoti shuleni tarehe……………..Mwisho wa kuripoti ni tarehe………………akiwa amekamilisha yale yote aliyoelekezwa katika fomu hii. Mustafa sabodo Sekondari ipo katika Halmashauri ya Wilaya ya Mtwara katika Mkoa wa Mtwara. Kwa wanaotoka mikoani kupitia Dar es Salaam usafiri wa kuja Mustafa Sabodo unapatikana kituo kikuu cha mabasi cha Magufuli au Temeke Mwisho, uliza mabasi yaendayo Mtwara na shuka Shuleni Mustafa Sabodo maana Shule iko barabarani. Kwa walioko mikoa ya Nyanda za Juu Kusini watatumia usafiri wa barabara kupitia Songea, Tunduru hadi Masasi, mnazi mmoja na kufika Mustafa Sabodo. Shule ina mazingira mazuri na huduma zote muhimu zinapatikana kwa uhakika.

Karibu sana Mustafa Sabodo Sekondari.

## MAELEKEZO/MAAGIZO NA MASHARTI YA KUJIUNGA NA SHULE

Ili mwanao apokelewe shuleni, anatakiwa afanye yafuatayo:-

Awasilishe hapa shuleni fomu “request for medical Examination” iliyojazwa na daktari yeyote wa hospitali ya serikali baada ya kupimwa. Fomu hiyo iambatanishwe na barua hii.

Afike na hati ya matokeo yake ya kidato cha nne (Result slip), nakala ya cheti cha kuhitimu kidato cha nne (Leaving certificate), nakala ya cheti cha kuzaliwa na namba ya NIDA kwa wanafunzi waliofikisha umri wa miaka 18.

### SARE YA SHULE

(i) Awe na sketi mbili nzito (cotton) rangi ya Ugoro (tobacco) rinda box na ziwe NDEFU hadi mwisho wa ugoko (ufundo) wa mguu

(ii) Shati mbili nyeupe (tetron) mikono mifupi, au kwa Waislamu nusu kanzu mbili nyeupe zisizobana za mikono mirefu

(iii) Kwa Waislamu Juba (kijuba) mbili rangi nyeupe za kushonwa ifunike kifua cha mwanafunzi pia iwe ndefu kufikia kifundo cha mkono akisimama na kofia nyeupe ya kichwani

(iv) Awe na jozi mbili za viatu vya ngozi vyeusi vya kamba visigino vifupi.

(v) Awe na jozi mbili(2) au zaidi za soksi nyeupe, ziwe ndefu (Stoking)

(vi) **Gauni** mbili rangi ya dark blue nzito (cotton) rinda box na ziwe NDEFU hadi mwisho wa ugoko (ufundo) wa mguu kwa ajiri ya kushindia na kufanyia kazi za njee.

(vii) Tshirt 2 rangi ya kijivu ya kuiva (FORM SIX) **zenye nembo ya shule** kwa ajili ya kushindia na kazi za nje **zinapatikana shuleni** au nusu kanzu mbili (2) zisizobana za kijivu ya kuiva za mikono mirefu na juba mbili rangi ya kijivu za kushonwa na kofia ya kijivu.

(viii) Awe na nguo za ndani za kutosha pamoja na taulo za kike (pedi) za kutosheleza muhula mzima.

(ix) Kanga doti moja.

(x) Taulo la kuogea

(xi) Traki suti rangi ya bluu **(traki suti isiwe na kofia)**

(xii) Raba nyeupe kwa ajili ya michezo.

**MUHIMU SANA**: ***Nguo zingine tofauti na zilizoainishwa katika fomu hii haziruhusiwi na hivyo mwanafunzi hatakiwi kuja nazo shuleni.***

## MICHANGO MBALIMBALI YA SHULE

**Michango ya Shule**

| S/N | MCHANGO | KIASI |
|---|---|---|
| 1 | Uendeshaji wa shule | 65,000/= |
| 2 | Nembo | 5.000/= |
| 3 | Tahadhali | 5.000/= |
| 4 | Kitambulisho | 5,000/= |
| JUMLA | | **80,000/=** |

**NB:** ***Malipo yote yalipwe kupitia akaunti namba ya shule***

**Jina la akaunti ni: MUSTAFA SABODO SEKONDARI**

**Namba ya Account: 70601200110**

**Jina la Bank: NMB BANK**

**MAHITAJI MENGINE.**

(i) Godoro futi $2^1/_2$ x 6, kama ana changamoto ya kukojoa kitandani Godoro lake lishonewe **BED COVER.**

(ii) Chandarua rangi ya bluu ya pembe nne.

(iii) Awe na daftari kubwa (counter book 2Q au 3Q) za masomo 8.

(iv) Aje na kadi ya mfuko wa Matibabu/BIMA KUBWA Au aje na Tsh. 52,000 kwa ajiri ya kutengenezewa bima ya Afya ya Mfuko wa NHIF shuleni.

(v) Vifaa kwa ajili ya kuwekea chakula. (kijiko,kikombe na kontena lenye vyumba)

(vi) File mbili.

(vii) Sanduku imara la chuma la kuweka vitu vyake.

(viii) Shuka mbili rangi ya pink

(ix) Sweta 1 rangi ya ugoro.

(x) Tochi ya kumsaidia wakati umeme ukikatika.

(xi) Taulo ya kuogea.

(xii) Rimu za karatasi Nyeupe bunda mbili (2) kwa mwaka (**kampuni ya aone. Ina kava jekundu**) Ndoo ndogo mbili zenye mfuniko, Kwanja moja, Panga moja lililo nolewa, Jembe moja lenye mpini, Fagio mmoja wa ndani (soft broom), Fagio moja ya nje (Chelewa), Dawa ya kusafishia choo lita 5 na Hard bloom moja (ya kusafishia au kusugulia chooni).

[ **Ukipenda unaweza kununua shuleni vitu vifuatavyo ;- Shuka, Vyombo vya kulia chakula, Daftari za counter book, Rimu, Fagio zote, Chandarua, Panga, Jembe, Kwanja, Ndoo, Dawa ya kusafishia choo, Hard bloom na Godoro. ]**

## ZINGATIA YAFUATAYO

i. Mwanao anapaswa asome sheria, kanuni na taratibu za shule, na kama yuko tayari kufuata taratibu husika akiri mbele yako kwa kujaza fomu husika zilizoambatanishwa

ii. Mwanafunzi atakae chelewa kufika Shuleni zaidi ya tarehe……………….**hatapokelewa**. Hivyo ni vyema ukamwandaa mapema mwanao na akafika mapema Shuleni. Wanafunzi wa kidato cha tano wataanza kuingia darasani na kufundishwa tarehe… … … … … **,** aidha watafanya mtihani/jaribio la kwanza kuanzia tarehe… … … … … . . mpaka tarehe……………..

iii. **SI RUHUSA** kwa Mwanafunzi kumiliki **SIMU** awapo Shuleni na endapo atabainika/atakamatwa na **SIMU** atasimamishwa/atafukuzwa Shule.

*Tafadhali, mwanafunzi afike Shuleni na barua hii na ajaze kwa ukamilifu sehemu ya taarifa zote maalum.*

*Nakutakia safari njema*

## SHERIA ZA SHULE

Zifuatazo ni sheria za Shule kinyume nazo kutasababisha Mwanafunzi kuadhibiwa, kusimamishwa masomo au kufukuzwa Shule kabisa

### MAKOSA YA KUFUKUZWA SHULE

1. Wizi
2. Uvutaji wa sigara
3. Kupata ujauzito au kutoa mimba.
4. Uasherati, uhusiano wa jinsi moja, kuoa au kuolewa
5. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro
6. Kugoma na kuhamasisha mgomo
7. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla
8. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga Mwalimu au mtu yeyote kwa ujumla.
9. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yeyote yale yanayovunja sheria za nchi
10. Kudharau Bendera ya Taifa
11. Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni
12. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.
13. Wanafunzi wote hawatakiwi kufuga na kusuka **nywele** wakati wote wawapo Shuleni.
14. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya madawa ya kulevya.
15. Kutoka nje ya Shule bila kibali/ruhusa
16. Kukataa adhabu kwa makusudi.
17. Kumiliki, kukutwa au kutumia **SIMU** ya mkononi katika mazingira ya Shule.

***MAKOSA YATAKAYOSABABISHA MWANAFUNZI KUADHIBIWA:***

1. Kutumia lugha chafu dhidi ya wanafunzi wenzake, kwa walimu au mtu mwingine yeyote
2. Kutovaa sare sahihi
3. Kutowaheshimu wafanyakazi wote waliopo shuleni kama walezi wake.
4. Kutoonyesha dhamira ya kusaidia na kushiriki katika kazi kwani kazi ni kielezo cha utu

5. Kutoheshimu au kutothamini kazi za aina zote zinazotolewa na uongozi wa shule 6. Kuvaa mavazi yasiyo na heshima
7. Kutotii kengele au kushindwa kuitikia wito wa kiongozi aliyemuita
8. Kutoheshimu picha za viongozi wa Serikali, Nembo ya Taifa, Wimbo wa Taifa na Fedha za Taifa
9. Kutohudhuria vipindi vya darasani kwa muda wote wa masomo
10. Kushindwa kuthamini muda
11. Kutowahi katika shughuli zote kama zilizopangwa ukiwemo wito wa dharura
12. Kutohudhuria kazi zote za mikono, mikutano yote ya shule, ukaguzi na usafi
13. Kufuga nywele
14. Kutovaa sare za shule katika sehemu zifatazo
    a. Darasani
    b. Shughuli za kishule nje ya shule
    c. Mhadhara wa shule (school baraza)
    d. Kwenda kutibiwa hospitalini
    e. Kwenye maandamano yaliyo rasmi
    f. Anaposafiri kwenda na kurudi likizo
15. Kuvaa kofia, viatu vya gorofa na mapambo yeyote kwa mfano pete, mkufu.
16. Uchafu wa mwili na mavazi 17. Kutoheshimu mipaka ya shule.
18. Marufuku kuingia sehemu zifuatazo bila ruhusa
    a. Ofisi ya walimu
    b. Ofisi za shule
    c. Maabara
    d. Jikoni
    e. Nyumba za walimu na wafanyakazi wasio walimu

**REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION FORM.**

To be completed by a medical officer (NAME)…………………………………………………………………

Name of student……………………………………………………………………………………………
Form ………………………………………Term ……………………….. Year …………………………………

Dear Doctor

Please kindly examine the above named student to prove his/her fitness undertaking studies at our school.

1. X-ray ( ) 2. Urine ( ) 3. Stool ( )
4. Physical fitness ( ) 5. V.D ( ) 6. Tuberculosis ( ) 7. Pregnancy ( )

A: (I) PRELIMINARY INFORMATION BY THE STUDENT BEFORE THE DOCTOR)

| NO | DISEASE | YES/NO | NO | DISEASE | YES/NO |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Tuberculosis | | 10 | Epilepsy | |
| 2 | Pneumonia | | 11 | Ear, Nose and threat | |
| 3 | Asthma | | 12 | Skin disorder disease | |
| 4 | Heart trouble | | 13 | Anemia | |
| 5 | Recurrent indigestion | | 14 | Operations | |
| 6 | Jaundice | | 15 | Serious Accident | |
| 7 | Dysentery | | 16 | Malaria | |
| 8 | Kidney and Urinary trouble | | 17 | Stomach trouble | |
| 9 | Nervous breakdown | | 18 | Eye disorder. | |

**Official**

B: MEDICAL EXAMINATION REPORT

a. Weight
b. Heat Beat
c. Vision etc

**MEDICAL CERTIFICATE**

I have examined the above and consider that he/she is physically fit/unfit to undergo studies.

DOCTORS NAME:……………………………………….SIGNATURE ……………

***(Official stamp)***…………………..

STATION:……………………DATE ……….…………PHONE………………………

## TAARIFA MUHIMU KUHUSU MWANAFUNZI MPYA.

**PICHA**
……

**SEHEMU A.**

JINA LA MWANAFUNZI
……………………………………………………………………………………………

wa kidato cha ……….. Mchepuo wa ......................Mwaka
……………………………………….

Dini ……………………………………………………………………………………………………………….

**SEHEMU B: TAARIFA ZA WAZAZI/WALEZI NA JAMAA:**

(i) Baba anaitwa……………………………………………………………………………………………….

Anaishi kijiji/mtaa ………………………………………………………… kata ………………………………….

Kazi yake ni ……………………………………………………….. na anwani yake ni …………………………

Namba yake ya simu ni …………………………………………………………………………………………

(ii) Mama yangu anaitwa………………………………………………………………………………………..

Anaishi kijiji/mtaa ………………………………………………………… kata ………………………………..

Kazi yake ni ……………………………………………………….. na anwani yake ni …………………………

Namba yake ya simu ni ……………………………………………………………………………………………

(iii) Jina kamili la Mzazi/Mlezi anayemuhudumia mwanafunzi ikiwemo kumpatia mahitaji yake Muhimu

…………………………………………………………………………………………………………………

Uhusiano ……………………………………………………………………………………………………….

Anuani Kamili …………………………………………………………………………………………………

Simu ………………………………………………………… Barua pepe ……………………………………..

Kazi yake ……………………………………………………….. Umri ………………………………………….

(iv) Uwepo wa Wazazi: Baba – YUPO HAI/AMEFARIKI. Kama amefariki ni lini? …………………………………

Mama – YUPO HAI/AMEFARIKI. Kama amefariki ni lini? ……………………………………..

(v) Majina na picha za watu wasiozidi watatu watakaoruhusiwa kumtembelea mwanafunzi

**PICHA 1**

PICHA 2

PICHA 3

Jina Jina ………………………………… Jina ……………………………… Jina ……………………………….

uhusiano …………………………….. .. uhusiano …………………………….. uhusiano ………………………….

Simu ………………………………….. Simu ……………………………….. Simu ……………………………..

Mimi ..........................................................................................................ambae ni mwanafunzi wa kidato cha V /VI mchepuo wa ………………………………… katika mwaka wa masomo...........................................nathibitisha kuwa maelezo yote niliyoyatoa hapo juu ni ya kweli na sahihi.

**MUHIMU SANA: Passport size ya mwanafunzi itakayowekwa katika form hii, mwanafunzi apigwe akiwa amevaa shati jeupe la shule na nyuma kuwe na background ya kitambaa chenye rangi ya Blue bahari.**

**SEHEMU C: UTHIBITISHO WA MWANAFUNZI**

Mimi .............................................................................................nakiri kuwa nimezisoma sheria, kanuni na taratibu za shule kwa umakini na utulivu kubwa. hivyo basi ninaahidi "nitazifuata sheria, kanuni na taratibu za Shule kama zilivyoelekezwa. Aidha ninaamini kuwa sheria na taratibu zote zipo kwa nia ya kunisaidia katika Nyanja zote muhimu ikiwa ni pamoja na nidhamu na taaluma"
kinyume na hivyo hatua stahiki za kinidhamu zichukuliwe dhidi yangu

jina la Mwanafunzi ……………………………………………………….. sahihi ……………………………………
jina la mzazi/mlezi …………………………………………………….. Sahihi …………………………………..
Tarehe……………………..

***N:B Mwanafunzi aje na vitabu kwa mujibu wa tahsusi yake na itakuwa ni mali yake.***

**ORODHA YA VITABU**

**GENERAL STUDIES**

1. Genera studies supplementary books for advanced level and colleges
2. Understanding General Studies For Advanced level By Joannes Bigirwamungu,Sospeter M,Deogratias, 2018)
3. Contemporary approach for Advanced level studies notes for form V&VI. Nyambari Nyangwine

**ENGLISH LANGUAGE**

1. Advanced level English language 1 form 5 & 6. Shadrack G.Ndambo
2. The real English textbook for advanced level. Dr. Kadeghe Michael
3. Advanced English Language 1 form 5 and 6. Oxford
4. English language paper 2. Nicholous Asheli
5. English language paper 2. Nyambari Nyangwine
6. Advanced Level English Language Structure & Stylistics. Nicholous Asheli
7. The Comprehensive Linguistics. Mgonja, M.E
8. Linguistics Concepts for Advanced Learners. Julton Sanga

**READINGS**

1. A Man of the People. Chinua Achebe
2. The Beautiful Ones Are Not Yet Born. Ayi Kwei Armah
3. His Excellency the Head of State. Danny Sado
4. Betrayal in the City. Francis Imbuga

5. Black Mamb John Ruganda
6. Lwanda Magere. Okoiti
7. The Bride Austin Bukenya
8. The woundrful surgen and the poems by Charles Mloka
9. I Will Marry When I Want. Ngugi wa Thiongo & Ngugi wa Mirii
10. An Enemy of the People. Henrisk Ibsen
11. Selected Poem. Institute of Education
12. The wonderful Surgeon and other Poems. Charles Mloka
13. Encounters from Africa by macxmillian educ .Ltd
14. Vanishing shadows by Namige Kyando
15. A season of waiting by david omewale
16. Rape of the peart by
17. Literature in English Advanced level by Nicolas Asheri

**HISTORY**

1. Shibitari. History 1&2
2. Salehe Yasini. History 1&2
3. Bakari Madaya.History1&2
4. Major events. History 1&2

**KISWAHILI**

Kiswahili kidato cha V na VI (TIE)
Kiswahili kidato cha V na VI (saluhayo)
Misingi ya Fasihi ya Kiswahili KIDATO CHA Tano na Sita by Gwivaha G.J

**A. RIWAYA**

1. Vuta Nkuvute
2. Mfadhili
3. Usiku Utakapo Kwisha
4. Kufikilika

**B. TAMTHILIYA**

1. Morani
2. Kivuli kinaishi
3. Nguzo mama
4. Kwenye ukingi wa thim

**C. USHAIRI**

1. Fungate la Uhuru
2. Kimbunga
3. Mapenzi Bora
4. Chungu Tamu

**D. GEOGRAPHY**

1. Comprehensive approach to Physical Geography by Msabila.
2. Integrated Human Geography by Msabila (Geography 2)
3. Msabila Physical & Practical Geography
4. Practical Geography alive by Zist kamili.
5. Geography for Secondary Schools Form Five by TIE
6. Geography,an integrated Approach by David Waugh

E. **ADVANCE MATHEMATICS**

1. Pure mathematics 1& 2 by J.K. Back

House 2.Understanding Mathematics

3. Advanced Mathematics 1 & 2 by S. Chads
4. Mathematics: The core Course for A- level By Bostock
5. Mathematics By C.J.Tranter

**F. BASIC APPLIED MATHEMATICS**

1. Basic Applied Mathematics for Advanced Secondary Schools Form Five and Six by Septine I. Sillem
2. Basic Applied Mathematics for Advanced Secondary Schools Form Five and Six by TIE

**E. ECONOMICS**

1. Economics 1 & 2 by Tayebwa Mgisha
2. Modern Economics Theory by Dewelt
3. Modern Economics 20th Edition by Ahuja
4. Essential Economics 1 & 2 by Odhiambo
5. Comprehensive of Economics Questions and Answers by Tayebwa.

NB: karatasi zote zilizoambatanisswa katika fomu hii zisomwe, kufanyiwa kazi na zirejeshwe shuleni wakati wa kulipoti.

**Kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambae ni mwanafunzi ni mgonjwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa.**

*TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZILIZOPO HAPO JUU*

KARIBU SANA

**MKUU WA SHULE**